

Mabadiliko ya Utambulisho wa Mwanamke na Uimarishaji wa Ujinsuke: Mifano kutoka Riwaya ya Nyuso za Mwanamke (Mohamed, 2010)

Ernesta S. Mosha¹

Ikisiri

Tafiti mbalimbali kuhusu riwaya ya Kiswahili zinaonesha kuwa mwanamke amesawiriwa kwa mitazamo mbalimbali, ukiwamo mtazamo hasi. Usawiri wa mtazamo huo unamtambulisha mwanamke kama kiumbe dhaifu na duni. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Udenguzi, makala imeonesha namna mhusika mwanamke anavyoweza kubadilisha utambulisho hasi na kujenga utambulisho chanya. Makala imetumia data kutoka katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) zilizopatikana kwa usomaji makini. Makala imeweka bayana nafasi ya riwaya ya Kiswahili katika kujenga utambulisho wa mwanamke unaoimarisha ujinsuke². Matokeo haya yanatokana na uumbaji wa wahusika wanawake wanaodengua kaida za jamii zinazomkandamiza mwanamke na kufichua mbinu zinazotumiwa na baadhi ya wanajamii kuendeleza ukandamizaji huo. Pia, umuhimu wa wanawake kujitambua na kujisimamia umewekwa bayana.

1.0 Utangulizi

Mabadiliko ya utambulisho wa mwanamke ni suala linalowashughulisha watafiti kutokana na umuhimu wake katika jamii, hususani katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuonesha uwezo walionao wanawake katika nyanja mbalimbali za maisha. Mabadiliko ya utambulisho wa mwanamke yanaweka wazi nafasi ya mwanamke kama mtu mwenye mchango katika jamii, anayeshiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo endelevu na kupinga mifumo ya unyanyasaji (Begum, 2016; Green, 2004). Kazi za kubuni zina mchango katika mchakato wa kubadilisha utambulisho duni wa mwanamke. Jambo hili linafanyika kwa kuwasawiri wahusika wanawake wanaopinga mila kandamizi zinazoendelezwa na jamii (Hurstons, 1990). Wahusika wa aina hii wanajengwa kwa namna ambayo wanakengeua mbinu za awali na kutoa nafasi ya utambulisho tofauti na ule

¹ Mhadhiri Mwandamizi, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe: emosha904@gmail.com

² Ujinsuke ni tafsiri ya neno *femininity* katika lugha ya Kiingereza.

uliozoeleka kwa muda mrefu. Ni dhahiri kuwa, waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaweza kuwajengea wanawake utambulisho unaokataa mila na tamaduni kandamizi na badala yake kuwajengea utambulisho mpya unaosisitiza usawa katika jamii. Kwa kutumia riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010), makala hii inaonesha umuhimu wa kuwa na wahusika wenye uwezo wa kuhoji mbinu mbalimbali zinazotumiwa na jamii kuendeleza utambulisho kandamizi kwa wanawake na badala yake kujenga utambulisho wa usawa hatua kwa hatua.

Kitendo cha kujenga utambulisho tofauti kupitia wahusika wa riwaya, kinaonesha kwamba masharti au kanuni za kujenga utambulisho wa mtu binafsi si za kudumu. Hivyo hivyo, tunaweza kueleza kuwa utambulisho wa wanawake katika jamii si kitu cha kudumu bali ni matokeo ya athari za utendaji wa aina mbalimbali za uundaji wa ujinsia. Butler (2006) anakwenda mbali zaidi anapoeleza kuwa uundaji wa majukumu ya kijinsia katika jamii unajenga utambulisho unaowatesa wanawake kutokana na taratibu za kijamii zinazowadunisha na kuwaheshimisha wanaume. Kutokana na misingi ya muda mrefu iliyowekwa na jamii, wanawake wanaogopa kutengwa na jamii endapo watapinga kufuata utambulisho kubalifu wa kiutamaduni. Hii inatokana na utamaduni wa jamii husika kuamua mambo yanayowahusu wanajamii, wanawake wakiwamo. Kwa kutumia kazi za bunilizi, ni wazi kuwa inawezekana kubadilisha utambulisho unaowanyima haki wanawake na kuwajengea utambulisho wa usawa na haki. Makala hii inaonesha namna wanawake wanavyoweza kupata utambulisho chanya kwa kutumia data kutoka katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010).

2.0 Nadharia ya Udenguzi

Katika kuchunguza namna riwaya ya Kiswahili inavyoweza kumjengea mwanamke utambulisho chanya, makala imeongozwa na Nadharia ya Udenguzi. Nadharia hii inaweka wazi kuwa ujuzi na maarifa si vitu vinavyoweza kueleweka kwa namna moja katika matini yoyote ile (Derrida, 1973). Kwa hiyo, tafsiri ya matini kwa wahakiki inaweza kuelezwa kwa namna tofauti, kila mhakiki akiwa na maana yake. Hii inaonesha kwamba, maana zinaweza kuendana au kupingana. Hivyo, kuna umuhimu wa kuchunguza matini ili yale yanayoeleweka kwa uwazi na ambayo hayapo wazi kwenye matini yaeleweke (Norris, 2002). Kwa upande wake Ntarangwi (2004) anaeleza kuwa Nadharia ya Udenguzi inasisitiza usomaji wa kina ili kuumba maana mpya na ya kipekee kutoka katika matini kwa kutumia vilongo vinavyomzunguka msomaji. Kwa hiyo, kwa kutumia nadharia hii, tunaweza kudadavua namna ambavyo wanawake wanaweza kuumba maana mpya ya utambulisho wao kupitia matini za riwaya ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Rorty (1996) anafafanua kuwa Udenguzi ni nadharia inayochunguza ukiushi wa kaida za jamii katika matini. Anafafanua kuwa ukiushi huu utokeapo kwa mara ya kwanza, huonekana kama ni usaliti. Hata hivyo, lengo la ukiushi husika ni kufikisha ujumbe fulani kwa walengwa. Rorty

(1996) anaongeza kuwa Derrida katika Nadharia ya Udenguzi anatoa mbinu mpya za kufichua yale yaliyoelezwa na waandishi kuhusu yanayoendelea katika jamii kwa uwazi. Ufafanuzi wa Rorty unatoa picha kuwa kwa kutumia Nadharia ya Udenguzi tunaweza kuchuguza ukiushi uliojitokeza kuhusu utambulisho uliozoeleka wa mwanamke katika riwaya teule. Kwa njia hii, Nadharia ya Udenguzi inatumiwa kuumba upya matini kwa lengo la kukidhi mahitaji ya wasomaji kwa wakati fulani.

Aidha, Nadharia ya Udenguzi inatumiwa na wahakiki kuchunguza mfumo wa jamii unavyoendeleza vilongo kandamizi katika jamii (Derrida, 1973). Katika kufanya hivyo, hatua ya kwanza ya wahakiki ni kujua mbinu gani zinatumiwa ili baadhi ya wanajamii waheshimike na wengine watwezwe. Hatua ya pili ni kuchunguza namna ambavyo kazi za kifasihi zinaweza kutumika ili kubadili mfumo kandamizi wa jamii. Kubadilisha mfumo kunaanza na kubadilisha namna ya kufikiri na kutenda ili kuleta mabadiliko (Green, 2004). Kufikiri kwa namna tofauti kunawapa nafasi wale wanaokandamizwa kujua kwamba kuna namna ya kupata yale wanayotamani katika maisha yao. Kwa hiyo, makala hii imetumia Nadharia ya Udenguzi kuchunguza namna riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (Mohamed, 2010) ilivyodengua utambulisho duni wa wanawake katika jamii na kujenga utambulisho bora.

3.0 Methodolojia

Makala hii imetumia riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* iliyoandikwa na Said A. Mohamed. Riwaya hii imeteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kutokana na wahusika wa kike waliosawiriwa katika riwaya hii kuweka bayana ugumu wa mwanamke kubadilisha utambulisho aliopewa na jamii yake. Ugumu huo unatokana na mila na desturi za mfumo wa jamii zinazowakuza tangu wakiwa watoto mpaka watu wazima (Green, 2004). Aidha, riwaya hii imemsawiri mhusika mkuu, Nana, kwa namna ambayo ameweza kushinda vilongo zoeleka³ vinavyomsawiri mwanamke kama mtu wa kushindwa pale anapokwenda kinyume na desturi za jamii.

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* ilisomwa kwa makini na sehemu zilizoonesha namna mwanamke anavyoweza kubadilisha utambulisho duni aliopewa na jamii kwa njia ya wazi au isiyo ya wazi zilinukuliwa. Pia, sehemu zilizobainisha mbinu zinazomkwamisha mwanamke kubadilisha utambulisho duni aliopewa na jamii zilinukuliwa. Ili kuimarisha mjadala, riwaya nyingine za Kiswahili zimetumika kwa ajili ya kushadidia hoja na kutoa mifano.

3.1 Muhtasari wa riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*

Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* imeandikwa na Said A. Mohamed na kuchapishwa na Longhorn Publishers Ltd mwaka 2010. Mhusika mkuu katika

³ Vilongo zoeleka ni tafsiri ya *dominant discourses* katika lugha ya Kiingereza.

riwaya hii ni Nana. Mhusika huyu anakabiliana na changamoto mbalimbali zinazotokana na mila na desturi za jamii yake ikiwa ni pamoja na kunyimwa uhuru na haki ya kufanya maamuzi kuhusu maisha yake. Aidha, Nana anapinga vikali mila na desturi kandamizi za jamii na anataka kupata uhuru kama binadamu. Katika riwaya hii mwadishi anaweka bayana mbinu zinazotumiwa na jamii kumjengea mwanamke utambulisho duni. Kwa upande mwingine, mwandishi anabainisha namna wanawake wanavyoweza kujitambua na kujisimamia ili kushinda mila na desturi za jamii zinazowanyima haki za msingi. Kwa namna ya pekee, mwandishi anaonesha jinsi mwanamke anavyoweza kubadilisha utambulisho duni aliopewa na jamii na kujenga utambulisho aula na wa usawa.

4.0 Mabadiliko ya Utambulisho wa Mwanamke katika Riwaya ya Kiswahili

Sehemu hii inajadili namna riwaya ya Kiswahili inavyosawiri mabadiliko ya utambulisho duni wa mwanamke uliozoeleka kwa kuumba utambulisho bora unaomthamini mwanamke katika jamii. Uumbaji huu unatokana na uwezo wa mtunzi kuyachunguza na kuyaelewa kwa undani mazingira na ulimwengu unaomzunguka (Mohamed, 1995).

4.1 Kubadilisha Mila na Desturi Zoeleka kuhusu Wanawake

Katika kujenga utambulisho bora wa mwanamke, Mohamed (2010) amedengua kaida zilizozoeleka katika riwaya ya Kiswahili kwa kumuumba mhusika mwanamke anayejitambua na kujisimamia. Ujasiri wa mhusika mkuu Nana, umemwezesha kutambua kuwa kujitegemea ni jambo muhimu na ni lazima aanze kujitegemea mapema kama nukuu ifuatayo inavyoonesha:

Miaka ya mwanzo nilikuwa nikipelekwa na kurudishwa nyumbani kutoka shule kwa gari mojawapo miongoni mwa yale yaliyoendeshwa na madereva wetu. ... Lakini ghafla nilikataa kupelekwa shule na kurudishwa kwa gari. Nilikataa na kumwambia baba kwamba mimi si mtoto mchanga tena. Nilikuwa nataka kujifunza kuwa peke yangu na dunia yangu. Baba alikasirika sana. Akaniambia wazi kwamba bado mimi ni mwanagenzi wa dunia. Tena mimi ni mwanamke (Mohamed, 2010: 38).

Katika nukuu hapo juu, mwandishi anaweka wazi ujasiri wa mhusika Nana wa kumweleza baba yake kuwa anataka kujifunza kujitegemea na anaweka wazi kuwa yeye 'si mtoto mchanga'. Ingawa baba yake anakasirika na kueleza kuwa binti yake bado ni 'mwanagenzi wa dunia' na ni 'mwanamke', Nana anafanikiwa kuanza kujitegemea. Kufanikiwa kwa Nana haikuwa kazi rahisi bali kunatokana na kuweka msimamo na nia ya kuusimamia. Hii inaelezwa wazi na mhusika Nana anaposema:

Nilikataa katakata kuchukuliwa kwa gari, kwa hiyo niligoma kwenda shule. Pia, niligoma kula. Mpaka baba alipoona sio mchezo tena, ndipo

alipoamuru niende shule kwa gari lakini nirudi kwa miguu (Mohamed, 2010: 39).

Kutokana na kutambua kuwa ‘uhuru’ ni haki yake ya msingi, Nana anafanikiwa kuwa huru ingawa kwa kiasi. Ukiushi aliouonesha mwandishi kwa kumuumba mhusika mtoto wa kike anayefanikiwa kuwa huru ni mabadiliko katika usawiri wa wahusika watoto wa kike katika riwaya nyingi za Kiswahili. Mathalani, katika riwaya ya *Utengano* (Mohamed, 1980) mhusika Maimuna ambaye ni mtoto wa kike kama Nana hakuruhusiwa na baba yake kutoka nyumbani. Alipochoka maisha ya kufungwa kama mtumwa na kutoroka, baba yake alikasirika sana, hivyo, kumwadhibu Bi. Tamima, mama yake Maimuna, kwa kuwa hakumlinda binti yake asitoke nyumbani peke yake.

Katika harakati za kuleta mabadiliko ni muhimu kuelewa namna mfumo unavyofanya kazi ili kuweza kupata mbinu anuwai za kufanya mabadiliko (Derrida, 1973). Matini za riwaya teule, zimeweka bayana namna vilongo zoeleka vinavyowakwamisha wanawake kwa kutowapa sauti za kuhoji yanayopangwa na jamii kuhusu wanawake. Mathalani, tafiti zinaweka bayana namna watoto wa kike wanavyolazimishwa kuolewa na mateso wanayokutana nayo baada ya kuolewa (Michael na Weaver, 2003; Mosha, 2013). Kinyume na tafiti tangulizi ambazo watoto wa kike hawapewi nafasi ya kuhoji maamuzi ya wazazi, nukuu ifuatayo inaonesha mhusika Shemsa akihoji umuhimu na nafasi ya ndoa kwa watoto wa kike, anasema:

... kwa nini wazazi wangu wanaiweka mbele ndoa kuliko maisha na mustakabali wangu? Kwa nini wanaiweka mbele [ndoa] kuliko kazi yangu ya uuguzi niliyomaliza kuisomea juzijuzi tu? Kwa nini wanaiweka mbele arusi kuliko hiari yangu? Mimi nilikuwa na hakika kwamba kwa aina ya mume anayetaka kunioa ningekuwa mtawa tu. Nisingeliruhusiwa kufanya kazi niliyoisomea kwa juhudi na kutazamia kupata kipato changu mwenyewe ambacho kingenipa uhuru na kuniwezesha kujitegemea kwa namna fulani. Kwa nini nirolewe na kubaki kumtegemea mwanamume kwa ukamilifu? Kumtegemea bila kujua mwanamume mwenyewe atakuwaje kwangu? (Mohamed, 2010: 209 -210).

Katika nukuu, mwandishi amempa ‘sauti’ mtoto wa kike kuhoji vilongo vinavyosisitiza mtoto wa kike kuolewa. Pia, mtoto wa kike anahoji wazazi kuthamini ndoa kuliko maisha, kazi na hata utayari na ukubalifu wa mtoto kuolewa. Aidha, mwandishi anaweka wazi madhila ambayo mtoto wa kike anaweza kukutana nayo pindi anaposisitiziwa kuolewa badala ya kufanya kazi. Jambo muhimu analobainisha mwandishi ni mtoto wa kike kujitambua na kuelewa kuwa anatakiwa kujisimamia katika maisha yake na siyo kuwa tegemezi. Katika kulisisitiza hilo, mtoto wa kike anahimizwa kuhakikisha kuwa

anapata kipato ili aweze kujitegemea. Kuthamini kazi na kujitegemea ni mabadiliko ya utambulisho wa mtoto wa kike yanayoelezwa na mwandishi. Cornwall (2016) anasisitiza kwamba, utambulisho wa wanawake unaojiegemeza kwenye kujitegemea utawasukuma wanawake wajitambue na kujisimamia badala ya kuongozwa na vilongo zoeleka.

Ni dhahiri kuwa kujitambua na kujisimamia kutabadilisha mawazo yaliyojengeka katika jamii kuhusu mtoto wa kike kuwa ni mzigo tena usiofaa kwa familia, kama anavyoeleza mwandishi:

Tokea zamani wazazi waliona bora waondoe bidhaa mbovu njiani. Yaani mtoto wa kike ni bidhaa mbovu itakayokuja kuwaozea ndani huku wanaona. Mtoto wa kike akishakuwa mwari, basi kishakuwa mzigo au bidhaa mbovu kwa familia. Ni mtego kwa heshima ya familia nzima pia (Mohamed, 2010: 210).

Mwandishi anaonesha utambulisho duni aliokuwa nao mtoto wa kike kwenye jamii namna ulivyomtweza na hata kumdhalilisha. Kwa hiyo, kujenga utambulisho mbadala kutamwezesha mtoto wa kike kutambua kuwa yeye ana nafasi sawa na mtoto wa kiume katika jamii na siyo 'bidhaa mbovu'. Tafiti zinabainisha kuwa kuna faida nyingi kwa jamii zinazotokana na mtoto wa kike kujitambua. Hii ni pamoja na kupata uwezo wa kuamua ni wakati gani wa kuingia kwenye mahusiano, kuanzisha familia na hata namna ya kuongeza kipato chake binafsi na familia (Hunt na Emma, 2016).

Katika kusisitiza umuhimu wa mabadiliko ya utambulisho wa mwanamke, mwandishi anamuumba mhusika Nana na kumpa ujasiri wa kumkataa mchumba ambaye ametafutiwa na baba yake, anasema:

... nilikataa baba kunichagulia njia ya kupita au rafiki wa kufuatana naye ... Mimi [Nana] nilimkataa katakata Dusa awe mwenzi wa kuishi nami milele. Wa kulala naye kitanda kimoja. Dusa kijana mwenzangu ndiyo, lakini sikumchagua. Nimechaguliwa na babangu awe mchumba wangu na hatimaye mume wangu. Dusa kijana mtukutu. Babake ni kizito mwenzetu ndiyo, lakini... (Mohamed, 2010:44).

Vilevile, mwandishi anasisitiza umuhimu wa watoto wa kike kujitambua na kujua wanataka nini katika maisha. Mhusika Nana anaeleza:

Siku yangu ya kupenda itafika. Nitapenda tokea chini ya nyayo zangu mpaka utosini pangu. Sitataka kuchaguliwa kama alivyochaguliwa mamang'u. ... Sitahofu kusema nampenda jini yule. Sitahofu kusema simtaki malaika yule (Mohamed, 2010: 42).

Kupitia nukuu hizi ni dhahiri kuwa watoto wa kike wanahimizwa kujitambua na kukataa kulazimishwa na kufanyiwa mambo ambayo hawayataki. Nukuu zinaweka wazi kuwa mtoto wa kike anayejitambua anajua wazi kukubali kuolewa na kijana kwa sababu tu ni tajiri ilhali tabia yake hairidhishi, hakutakuwa na maana katika

maisha. Nukuu pia zinaweka bayana kuwa ni muhimu mtoto wa kike kuolewa na yule anayempenda pindi muda wa kuolewa ukifika. Hakika, uumbaji wa wahusika wa kike wa aina hii ni tofauti kabisa na msisitizo uliowekwa na riwaya tangulizi za Kiswahili kuhusu ndoa. Mathalani, katika riwaya ya *Shida* (Balisidya, 1975) mhusika Matika hakuweza kubishana na baba yake kuhusu mwenzi wa kumwoa. Otoo-Oyortey na Pobi (2003) wanaweka wazi kuwa katika nchi zinazoendelea suala la ndoa siyo la mjadala na watoto wa kike lazima wakubaliane na maamuzi ya baba zao. Kwa hiyo, kuwamba wahusika watoto wa kike wanaodengua kaida zoeleka unaanzisha mtazamo mpya kuhusu mtoto wa kike na hivyo kuanza kujenga fikra tunduizi kuhusu namna ambavyo wanaweza kujitegemea katika kufanya maamuzi. Jambo muhimu zaidi ni kuwa uandishi huu unaweka bayana ujasiri wa mtoto wa kike ambao unakinzana na ule wa vilongo zoeleka katika jamii. Aina hii ya uandishi unaelezwa na Davies (1992) kuwa unawasaidia wanawake kutambua mbinu zilizokuwa zinatumiwa na jamii kuwanyima haki zao za msingi na hata kuhoji vilongo zoeleka kuhusu nafasi ya kufanya maamuzi waliyonayo watoto wa kike na wanawake kwa ujumla. Ni wazi kuwa kujitambua na kujisimamia kama kulivyosawiriwa katika riwaya teule kunaonesha ujenzi mpya wa utambulisho wa mwanamke.

4.2 Ufusahi⁴ wa Kanuni za Ujinsia katika Riwaya ya Kiswahili

Usawiri wa wanawake katika kazi za fasihi unaonesha kuwa mwanamke anahimizwa kufuata mila na desturi za jamii yake hususani zile zinazoendeleza kanuni za ujinsia (Michael na Weaver, 2003; Mosha, 2013). Kanuni hizi zinaendeleza mtazamo kuwa wanawake ni raia wa ‘daraja la pili’, wanapolinganishwa na wanaume, hivyo, hawana ujuzi wa kufanya kazi za kitaalamu na wala hawawezi kufanya maamuzi ya busara (Musoke, 2005). Musoke anafafanua kuwa tabia hii ina mizizi kutokana na utawala wa kijamii unaoona kuwa wanaume wako juu ya wanawake. Hata hivyo, katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* tunaoneshwa kuwa wahusika wanawake wametambua msingi huu na wanakosoa kanuni hizi za ujinsia. Mhusika mkuu Nana anabainisha wazi jambo hili kupitia nukuu zifuatazo:

Maisha yetu wanawake hapa petu yamefinyangwa ndani ya tamaduni zilizoasisiwa na mwanamme ambazo bado zina nguvu kubwa kupita kiasi (Mohamed, 2010: 107).

Nikifumbua macho nikitazama kila upande ndani ya jamii yangu, huchukia mno tabia hii ya mwanamke kuwa mwanamke kwa namna mbalimbali zinazopangwa na mwanamme (Mohamed, 2010: 108).

⁴ Hili ni neno lililoundwa kutokana na kitenzi fusahi chenye maana ya ‘tangua, batilisha’ (TUKI, 2019: 137).

Kwa umahususi, baadhi ya mambo anayoyaeleza mhusika Nana kuwa yanapangwa na wanaume na kwamba ni lazima yakataliwe ni pamoja na kupangiwa mambo ya kufanya katika maisha kama anavyofafanua akisema:

... Babangu hakutaka niwe na rafiki kutoka nje. Hakutaka nishiriki mchezo wowote nje ya nyumba yetu. Hii ilikuwa ni njia yake ya kunizuia nisichafuliwe na ulimwengu wa nje. Anilee, au bora anifinyange kama anavyopenda kuwafinyanga wake zake (Mohamed, 2010: 118).

Katika nukuu hizi, mhusika Nana anaweka wazi kwamba maisha ya wanawake yanaratibiwa na wanaume. Anatoa mfano wa jinsi baba yake alivyomtenga na ulimwengu unaomzunguka. Kitendo cha kunyimwa kuwa na marafiki na kucheza na watoto wenzake nje ya nyumba, kinaonekana kumnyima Nana uhuru wa kujua yale yanayoendelea. Ingawa baba yake anaeleza kuwa nia ya kumfungia ni 'kumzuia asichafuliwe' na mambo ambayo hayataki. Pia, ni 'njia ya usalama' na 'yenye faida' kwa Nana. Hata hivyo, mhusika Nana hakubaliani na hali hii iliyojengeka katika jamii ya kumfungia mtoto wa kike ndani na kumwamulia mambo ya kufanya na kutofanya. Vilevile, nukuu zinaweka wazi kuwa maisha ya mwanamke yanaratibiwa na mwanamume ambaye anasimamia mila na desturi za jamii. Mwandishi kupitia mhusika Nana anaikemea tabia hii ya mwanamke kuamuliwa aweje. Ili kuondokana na hali hiyo, nukuu ifuatayo inaweka bayana kuwa ni vema mwanamke mwenyewe akaamua anataka nini katika maisha yake:

... [Nana] yeye ameshaamua. Yaani honne⁵ yake imemwamulia. Honne yake imeshaamua kwamba kiongozi wa kweli wa maisha yake ni nafsi yake mwenyewe, yaani ile sauti yake ya ndani kabisa (Mohamed, 2010: 161).

Tofauti na wahusika wa riwaya nyingi za Kiswahili, mhusika Nana anaweka bayana kuwa maisha yake yataongozwa na sehemu ya nafsi yake ya ndani *honne*. Suala muhimu hapa ni kuchunguza ni kwa nini mhusika Nana hakuchagua kuongozwa na *tatema*⁶ - sehemu ya nje ya nafsi yake, ambayo inaonekana na watu wanaweza kuitumia kumpima? Akifafanua kuhusu 'honne' na *tatema*, Mičková (2003) anaeleza kuwa *honne* inawakilisha hisia na mawazo ya kweli ya mtu ilhali *tatema* inawakilisha mawazo au mambo yanayokubalika kijamii. Kwa hiyo, pale ambapo mzungumzaji hataki kufichua hisia zake za

⁵ Hili ni neno la Kijapani likiwa na maana ya nafsi ya mtu ya ndani. Aina hii ya nafsi 'ndiyo inayotawala kuifanya dunia yake mtu na dunia ya watu wengine iwe njema au mbaya' (Mohamed, 2010: 161).

⁶ Hili ni neno la Kijapani likiwa na maana ya nafsi ya mtu ya nje. Aina hii ya nafsi 'ndiyo inayoonekana waziwazi. ... mtu hupimwa kwa *tatema* yake' (Mohamed, 2010: 161).

kweli kuhusu anayofikiri au anayotaka, basi anatumia *tatema*. Kutokana na ufafanuzi wa Mičková, ni dhahiri kuwa mhusika Nana hayupo tayari kufanya mambo yanayowaridhisha au kuwafurahisha wengine kutokana na mfumo wa jamii ilhali yeye mwenyewe anaumia. Kadhalika, anataka kuongozwa na yale yanayotoka ndani ya nafsi yake na si kulazimishwa kwa namna yoyote. Katika kusisitiza umuhimu wa jambo hili, Nana anaeleza:

Ukitaka kujua nini hasa sababu yangu ya ... kuota ndoto mpya au kubuni kisasili changu mwenyewe nitakuambia. ... Mimi ... licha ya kutotaka kubaki jikoni kupika na kupakua, kuosha vyombo na kufagia na kutunza watoto, sitaki mimi kamwe hata kuwa mwanamke kwa maana ya mwanamke anayetunzwa na kulindwa na mwanamme (Mohamed, 2010: 107).

Katika nukuu hapo juu ni wazi kuwa Nana anataka mambo mapya katika maisha yake; hataki kuongozwa na yale yaliyozoeleka katika jamii. Nukuu inasisitiza kuwa Nana si tu anakataa usaguzi wa kijinsia uliopanga kazi za wanawake, bali pia anakataa maana ya mwanamke kama inavyojulikana katika jamii – kutunzwa na kulindwa. Uumbaji wa wahusika wanawake wenye ujasiri wa kuhoji yale yaliyozoeleka katika jamii unawasaidia wasomaji wajue namna wanavyoweza kujinasua katika hali fulani wanayokutana nayo. Uumbaji huu unaendana na hoja ya Luke na Freebody (1997) wanapoeleza kuwa riwaya inaweza kuunda matini inayojenga ulimwengu unaowezekana na kuwaweka wasomaji katika nafasi ya kutafsiri ulimwengu huo kwa namna inayofaa kwao. Hii ina maana kwamba wasomaji wanapopata fursa ya kusoma taarifa tofauti na walizozoea wanapata njia mbadala za kuishi na wanaweza kugundua mbinu mpya za kukabiliana na maisha ya kila siku (Cullina, 2000; Ledbetter, 1996). Aidha, uzoefu huo unawasaidia kugundua uwezo na nguvu walizonazo katika kuleta mabadiliko. Halikadhalika, ili kuleta utambulisho bora wa wanawake, ni muhimu kuwa na wahusika wanaoazimia kuleta mabadiliko kutoka ndani kwa kuwa kama anavyoeleza Enciso (2001) mtazamo wa kijamii katika matini sio tu unaathiri matendo ya wasomaji lakini pia huathiri matarajio yao. Kwa hiyo, kama matini ya riwaya inashadidia kuwakomboa wanawake, haina budi kuchochea mabadiliko ya utambulisho zoeleka unaowakandamiza wanawake katika jamii.

4.3 Kushinda Vikwazo vya Kijamii na Kupata Uhuru Binafsi

Katika kuleta mabadiliko ya utambulisho wa mwanamke kuna mambo mengi ya kufanya. Miongoni mwa mambo hayo ni kuelimisha watu ambao wanachangia katika kuendeleza utambulisho duni wa mwanamke. Lengo hasa ni kuwafanya wajue umuhimu wa kuwathamini watoto wa kike na wanawake kwa ujumla. Katika suala hili, ujumbe alioutoa mhusika Shemsa katika majadiliano ya namna ya kuwakomboa wanawake, unaweka bayana suala hili:

Nataka kila mtu anione. Anifahamu. ... Ndiyo, nasema kila mtu lakini nasema zaidi na wazazi na wazee: baba zetu, mama zetu, bibi zetu, babu zetu, shangazi, wajomba.... Hasa baba zetu wanaochukua madaraka makubwa ndani ya jamii zetu (Mohamed, 2010: 204).

Ujasiri aliuonesha Shemsha unafafanuliwa na Mulokozi (2017) anaposema kuwa katika harakati za kuwakomboa wanawake ni lazima vilongo zoeleka vijenguliwe ili kujengwa vipya vitakavyoleta dhima mpya kuhusu wanawake katika jamii. Nukuu hapo juu inaonesha kuwa ni lazima kila mmoja ahusike katika kubadilisha hali ya mtoto wa kike na mwanamke kwa ujumla. Ingawa nukuu imeweka mkazo kwa wahusika katika familia, jambo muhimu ni kuwa ushirikiano katika kubadilisha utambulisho duni wa mwanamke katika jamii ni jambo lisiloepukika. Hakika, maneno ya mhusika Shemsa, yanathibitisha madai ya Bent-Goodley (2005) kwamba ushirikiano wa wanajamii unaweza kusaidia si tu kukomesha ukatili dhidi ya wanawake bali pia kujenga upya thamani ya mwanamke. Bent-Goodley anasisitiza kuwa familia pana ya Kiafrika ni njia yenye nguvu katika kubadili mila na desturi kuhusu mwanamke. Hii ni wazi kuwa matarajio ya wanafamilia kuhusu mwanamke yakibadilika, mtoto wa kike na wanawake wenyewe wataweza kufikiri tofauti. Hata hivyo, ugumu wa jambo hili unaoneshwa na wasikilizaji ambao walishangaa ujasiri wa mhusika Shemsa kama nukuu ifuatayo inavyoweza wazi:

Waliokuwa wakimsikiliza na kumfahamu nini anasema, walitanzwa na uwazi wa maneno yake. Ilikuwa adimu kupatikana mwanamke aliyeweza kusema wazi namna hii katika jamii. ... Basi ikawa maneno aliyoyotoa Shemsa leo ni maneno ya mwanamke aliyejitolea (Mohamed, 2010: 205).

Katika kuleta mabadiliko, ujasiri ni jambo muhimu sana. Ujasiri wa mhusika Shemsa ulionekana kuwashangaza wengi. Ni dhahiri kuwa ili kubadilisha utambulisho duni alionao mwanamke, ni lazima kaida zoeleka zinazomtambulisha mwanamke zikiukwe ili kuwajengea wahusika uelewa wa kujua ni nani wanaowakwamisha katika maisha. Hoja hii inawekwa wazi na Rorty (1996) anapoeleza kuwa ili kuleta mabadiliko ni lazima yale yanayowakandamiza wanawake katika jamii yafichuliwe kwa uwazi. Kwa njia hii wanawake watajitambua na kuweza kuchukua hatua kama inavyoelezwa na mhusika Nana katika nukuu ifuatayo:

Ingawa nilikuja hapa kwa hamu ya kujitoa ukumbini, baada ya kuyasikia haya niliitazama kazi hii kwa kejeli kubwa. Mimi nilikuwa najiamini, na tena sikuwa na pupa ambayo ingenitia mtegoni mwa biashara. Nisingetaka kununuliwa. ... Nisingelitaka kuiuza nafsi yangu kiasi hicho. Sikutaka kulazimishwa jambo lolote. Sikutaka kulazimishwa nyimbo za kuimba - nyimbo za matusi na masimango, nyimbo za mipasho na rusha roho. Nilizidharau mno nyimbo hizo zisizo mwala wala muruwa (Mohamed, 2010: 144).

Katika nukuu hapo juu mhusika Nana anaeleza kuwa alikuwa tayari kufanya kazi ukumbini - kazi ya kuimba. Hata hivyo, hakuwa tayari ‘kulazimishwa jambo lolote’ ikiwa ni pamoja na nyimbo atakazoimba ukumbini. Katika simulizi imewekwa wazi kuwa mhusika Nana alikuwa amepewa masharti kadhaa na meneja wa hoteli ya Selwa baada ya kuimba vizuri katika mahojiano ya kupata kazi. Nana aliweza kufanya maamuzi hayo kwa sababu alikuwa ‘anajiamini’ hivyo hakuwa tayari ‘kuiuza nafsi’ yake au ‘kununuliwa’ kwa namna yoyote.

Akiendelea kuonesha umuhimu wa kujitambua na kujisimamia, mwandishi anaweka wazi kuwa, mhusika Nana ana upeo wa kuamua aina ya maisha anayotaka hata pale anapoelezwa kuwa maisha hayo yamejaa mateso. Haya yanabainika pale ambapo Bimkubwa anamweleza Nana kuhusu maisha ya ndoa na kusema:

... Unataka kuolewa, hujui kwamba kuolewa ni kudhibitiwa na mwanamme? Umetoka kwenye balaa la babako kukudhibiti kama alivyotaka ... sasa umeingia katika mikono ya udhibiti ya mwanamme mwingine asiye babako wala mtu wako (Mohamed, 2010: 287).

Kutokana na ushauri uliotolewa na Bimkubwa kuwa ndoa ni maisha ya udhibiti na maisha yasiyokuwa na uhuru, mwandishi anatoa maoni yake kwa kusema:

Kwa nini mtu mwingine awe na haki ya kumchagulia furaha ya kutoolewa au msiba wa kuolewa? Nana ameshaona vya kutosha faida na hasara za vitu vyenye uzito, thamani, mng’aro wa kupendeza, fahari na heshima kwa mwenye navyo.... Kwenye ndoa zipo shida ndiyo - si uwongo, lakini shida ndiyo mbolea ya furaha. ... Hatimaye Nana ameamua, potelea mbali, atazama kwenye ndoa kwa kutaraji kuibuka kwenye ndoa, si kuzama tu moja kwa moja (Mohamed, 2010: 294).

Nukuu hii inaendelea kudhihirisha kuwa inawezekana tukawa na wahusika wanawake wanaoweza kuwa na utambulisho tofauti na ule uliozoeleka katika jamii. Kutokana na kujitambua, mhusika Nana ameweza kufanya maamuzi bila kulazimishwa au kupangiwa na mtu yeyote. Uwezo wa kufanya maamuzi ni muhimu sana katika mchakato wa kubadilisha utambulisho uliozoeleka katika jamii kuwa mwanamke hawezi kufikiri wala kufanya maamuzi faafu hata pale anapona kuwa jambo fulani litamfaa au halitamfaa katika maisha yake. Mwonoulimwengu mbadala unawasaidia wanawake kujitambua na kujua kuwa wao wenyewe wana nafasi ya kufanya maamuzi ya nini cha kufanya na maisha gani yanawafaa (Gardiner, 1981; Hayawaka, 1990; Howard, 2011).

4.4 Nguvu Anuwai na Utambulisho wa Mwanamke

Tafiti zinaonesha kuwa wanawake wenye uelewa kuhusu nguvu mbalimbali wanazokumbana nazo katika maisha wanaweza kujisimamia na kufanya maamuzi wanapokabiliana na changamoto (Dingley na Roux, 2014; Smith, Dingley na Roux, 2019). Kwa upande wao, Dingley na Roux wanafafanua kuwa wanawake

wanapotambua uwezo wa nguvu yao ya ndani wanaweza kujenga utambulisho kulingana na matakwa yao na si ya jamii inayowazunguka. Hii inaonesha kuwa nguvu ya ndani ina nafasi kubwa ya kuwafanya wanawake wabadilike ndani kwanza na mabadiliko hayo ndiyo yanayoonekana kwa nje kama anavyosimulia mhusika Nana:

... zaidi amegeuzika nafsi yake ya ndani si ya nje. Na nafsi yake ya ndani ilipogeuzika, alianza kugeuza vitu vyote na mambo yote yaliyohusiana na maisha yake. Na vitu vilipokubali kugeuzika, ikawa amegeuza maisha yake yote (Mohamed, 2010: 220).

Nukuu hapo juu inaweka wazi kuwa baada ya nafsi ya ndani kubadilika iliweza kubadilisha maisha ya nje. Tafsiri yake ni kuwa jambo muhimu zaidi ni nafsi ya ndani ya mhusika kukubali kubadilika. Mabadiliko ya ndani ndiyo yanayoleta athari chanya na ya kudumu (Mičková, 2003). Mičková anafafanua zaidi kuwa nafsi ya ndani inampa mtu uhuru wa kuishi kama anavyotaka, hivyo, kuhakikisha kuwa anapata mazingira ya kufanikisha jambo analokusudia kutoka ndani ya nafsi yake.

Kwa upande mwingine, mhusika Nana anaonesha umuhimu wa kujua nguvu zinazoweza kumkwamisha mwanamke katika shughuli zake za kila siku, anasema:

... kuna nguvu fichizi ambazo zinakulazimisha kuishi maisha usiyotaka. Hutaki kujiuza lakini unashikwa mkono kupelekwa sokoni kuuzwa ukitaka usitake ... Unataka kujinusuru, lakini unaambiwa jiue. Unataka uuhami mji wako unalazimishwa kuuangamiza. Unatakiwa kwenda uchi. Na wewe hutaki kwenda uchi, lakini unalazimishwa kuamini kwenda uchi ni vizuri (Mohamed, 2010: 221-222).

Kupitia mhusika Nana wanawake wanapewa tahadhari ya nguvu ambazo si rahisi kuzijua ila zipo na zinamlazimisha mwanamke kufanya jambo ambalo hataki. Katika nukuu, kuna nguvu fiche zinazolazimisha mwanamke kufanya mambo ambayo kwa nguvu ya ndani hataki lakini kwa nguvu ya nje analazimika kufanya. Akifafanua kuhusu nguvu za nje, Mičková (2003) anaeleza kuwa nguvu hizi zina msukumo mkubwa kwa mhusika na kwa kuogopa kwenda kinyume na matakwa ya wengi, mhusika hujikuta amefanya mambo ambayo kwa nguvu ya ndani asingefanya. Kwa hiyo, kutokana na mvutano wa nguvu fiche za nje, ni muhimu sana wanawake wakaimarisha nguvu ya ndani ili waweze kufanya maamuzi sahihi katika maisha.

Aidha, riwaya teule imeweka bayana mbinu faafu za kukabiliana na changamoto zinazoweza kutokea endapo mwanamke atafanya tofauti na yale yaliyozoeleka katika jamii kama nukuu inavyoeleza:

Hakuna funzo zuri kama la kuishi na kutambua nini kinatokea. Kujua hivyo ni hatua ya mwanzo ya kuendelea, hatua ya kuondoa hofu na kusitasita (Mohamed, 2010: 221).

Nukuu inaonesha wazi kuwa unapojiandaa kwa jambo linaloweza kutokea, inakusaidia kuondoa wasiwasi na kuwa na ujasiri wa kujaribu. Hali hii ilikuwa dhahiri kwa mhusika Nana. Katika riwaya teule imeelezwa kuwa Nana kwa kutambua hatari zinazoweza kutokea katika biashara zake, aliweka bima kwa rasilimali zake zote. Kwa hiyo, Ngware kaka yake Nana alipochoma moto jengo lake la biashara baada ya kutumwa na Bwana Hila, baba yake Nana, Nana hakukwama kibiashara badala yake alikuwa na biashara kubwa zaidi baada ya kupokea malipo ya mali zilizoungua moto. Uumbaji huu wa mhusika mwanamke anayeshinda vikwazo mbalimbali ni tofauti na riwaya nyingi za Kiswahili ambazo zinaonesha kuwa mtoto wa kike anapokwenda kinyume na matakwa ya baba yake anaishi maisha ya shida. Mfano mzuri ni mhusika Maimuna katika riwaya ya *Utengano* na Matika katika riwaya ya *Shida*. Ni dhahiri kuwa uumbaji wa mhusika Nana umedengua kaida zoeleka, hivyo, kunawapa wasomaji hasa wanawake namna bora ya kukabiliana na masuala yanayowakwamisha katika jamii.

5.0 Hitimisho

Makala imeonesha kuwa riwaya ina nafasi ya kubadilisha utambulisho duni wa mwanamke na kujenga utambulisho bora. Hii inatokana na riwaya kuchochea namna tofauti ya utendaji kwa watoto wa kike na wanawake. Aidha, riwaya zinazotoa mwelekeo wa namna ya kubadilisha utambulisho duni wa mwanamke katika jamii, zipo kwenye nafasi nzuri ya kuweka bayana mchango wa mwanamke katika jamii. Pia, riwaya za aina hii zinaweza kutumika kama njia mbadala ya kuchochea na kuendeleza mawazo kuwa wanawake wana nafasi sawa na wanaume katika kuchangia maendeleo ya jamii (Gardiner, 1981; Weedon, 1997; Green, 2004; Mosh, 2017). Hata hivyo, ili wanawake waweze kuwa na utambulisho bora, ni muhimu kujua mbinu zinazotumiwa na mfumo wa jamii kuwadunisha na namna unavyoendelezwa katika jamii husika (Derrida, 1973). Katika makala hii, mjadala umeweka bayana mbinu anuwai zinazotumiwa na jamii kuhakikisha wanawake wanabaki katika nafasi duni. Pia, makala imeonesha namna wahusika walivyokabiliana na changamoto walizokutana nazo. Vilevile, makala imejadili namna ukiushi wa kaida za jamii (Rorty, 1996) zinazowakandamizi wanawake unavyosaidia katika kuleta mabadiliko ya utambulisho. Katika makala hii, uumbaji wa wahusika wanawake waliodengua kaida zoeleka zinazowakandamiza, ni mbinu ya kujenga utambulisho bora na kuimarisha ujinsuke. Kwa hiyo, waandishi wa riwaya wanapowasawiri wahusika wanawake wanaouelewa mfumo wa jamii na kuweza kutangua yale yanayowadunisha, wanachangia kujenga utambulisho bora kwa wanawake. Utambulisho huu unawawezesha wanawake kujitambua, kujiamini na kujisimamia katika maisha yao ya kila siku.

Marejeleo

- Balisidya, N. (1975). *Shida*. Nairobi: Foundation Books.
- Begum, H.S. (2016). "Deconstruction of Gender Identities: A study of the Novels of Nwapa, Emecheta and Adichie". *Journal of English Language and Literature*. 3(1): 86-93.
- Bent-Goodley, T.B. (2005) "Culture and Domestic Violence: Transforming Knowledge Development". *Journal of Interpersonal Violence*. 20(2): 195-203.
- Butler, J. (2006). *Gender Trouble: Feminism and the Subversion of Identity*. New York: Routledge.
- Cornwall, A. (2016). "Women's Empowerment: What Works?" *Journal of International Development*. 28(3): 342-359.
- Cullinan, B. (2000). "Independent Reading and School Achievement". *School Library Media Research*. 3: 1-24.
- Davies, B. (1992). "Women's Subjectivity and Feminist Stories". Katika C. Ellis na M.G. Flaherty (Wah.), *Investigating Subjectivity: Research on Lived Experience*. England: Sage. Kur. 53-76.
- Derrida, J. (1973). *Speech and Phenomenon*. Evanston: Northwestern University Press.
- Dingley, C. na Roux, G. (2014). "The Role of Inner Strength in Quality of Life and Self-Management in Women Survivors of Cancer". *Research in Nursing and Health*. 37: 32-4.
- Enciso, P.E. (2001). "Taking our Seats: The Consequences of Positioning in Reading Assessments". *Theory into Practice*. 40(3): 166-174.
- Gardiner, J.K. (1981). "On Female Identity and Writing by Women". *Critical Inquiry*. 8: 347-361.
- Green, M.C. (2004). "Transportation into Narrative Worlds: The Role of Prior Knowledge and Perceived Realism". *Discourse Processes*. 38(2): 247-266.
- Hayakawa, S.I. (1990). *Language in Thought and Action*. New York: Harcourt Brace.
- Howard, V. (2011). "The Importance of Pleasure Reading in the Lives of Young Teens: Self-identification, Self-construction and Self-awareness". *Journal of Librarianship and Information Science*. 43(1): 46-55.
- Hunt, A. na Emma, S. (2016). *Women's Economic Empowerment: Navigating Enablers and Constraints*. London: Overseas Development Institute.
- Hurston, Z.N. (1990). *Their Eyes were Watching God*. New York: Harper and Row.
- Ledbetter, M. (1996). *Victims and the Postmodern Narrative or Doing Violence to the Body: An Ethic of Reading and Writing*. New York: St. Martin's Press.
- Luke, A. na Freebody, P. (1997). "Shaping the Social Practices of Reading: Reading and Colonization". Katika S. Muspratt, A. Luke na P. Freebody

- (Wah.), *Constructing Critical Literacy: Teaching and Learning Textual Practice* Cresskill, New York: Hampton Press. Kur. 185-225.
- Michelle, C. na Weaver, C.K. (2003). "Discursive Manoeuvres and Hegemonic Recuperations in New Zealand Documentary Representations of Domestic Violence". *Feminist Media Studies*. 3(3): 283-299.
- Mičková, J. (2003). "The Japanese Indirectness Phenomenon". *Asian and African Studies*. 12(2): 135-147.
- Mohamed, S.A. (2010). *Nyuso za Mwanamke*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Mohamed, S.A. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili: Tamthiliya, Riwaya na Hadithi Fupi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Mohamed, S.A. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longman Publishers.
- Mosha, E. (2013). "Textual Construction of Domestic Violence: Examples from Kiswahili Novels". *Kiswahili*. 76: 45 -60.
- Mosha, E. (2017). "Uimarishaji wa Ujinsuke katika Fasihi ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Hadithi Teule za Kiswahili za Watoto". *Kioo cha Lugha*. 15: 158 -174.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Musoke, H.D. (2005). "Shattering the Glass Ceiling: What Women in Uganda Need to Make it to the Top". Katika J. Bond (Mh.) *Voices of African Women: Women's Rights in Ghana, Uganda, and Tanzania*. North Carolina: Caroline Academic Press. Kur. 366-378.
- Norris, C. (2002). *Deconstruction*. London: Routledge.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island: Augustina College.
- Otoo-Oyortey, N. na Pobi, S. (2003) "Early Marriage and Poverty: Exploring Links and Key Policy Issues". *Gender and Development*. 11(2): 42-51.
- Rorty, R. (1996). "Remarks on Deconstruction and Pragmatism". Katika C. Mouffe (Mh.) *Deconstruction and Pragmatism*: London: Routledge. Kur. 13-18.
- Smith, C.S., Dingley, C. na Roux, G. (2019). "Inner Strength—State of the Science". *Canadian Journal of Nursing Research*. 51:(1) 38–48.
- Weedon, C. (1997). *Feminist Practice and Poststructuralist Theory*. Oxford: Basil Blackwel.